

SWALI: Kaini baada ya kumuua ndugu yake Abeli, alikimbilia katika nchi ya Nodi, Naomba kufahamu Je! Huko alipatia wapi mke na kuzaa naye watoto? (Mwanzo 4:16).

**JIBU:** Ukisoma **Mwanzo 5:1-5** utaona inasema....

*“1 Hiki ndicho kitabu cha vizazi vya Adamu. Siku ile Mungu alipoumba mtu, kwa sura ya Mungu alimfanya;  
2 mwanamume na mwanamke aliwaumba, akawabariki akawaita jina lao Adamu, siku ile walipoumbwa.  
3 Adamu akaishi miaka mia na thelathini, akazaa mwana kwa sura yake, kwa mfano wake, akamwita jina lake Sethi.  
4 Siku za Adamu baada ya kumzaa Sethi zilikuwa miaka mia nane, AKAZAA WANA, WAUME NA WAKE  
5 Siku zote za Adamu alizoishi ni miaka mia kenda na the lathini, naye akafa.”*

Sasa kwenye Mstari huo wa 4 utaona kuwa kumbe mbali ya Kaini na Abeli kuzaliwa na Adamu kulikuwa na wana wengine wa kike na wakiume waliokuja kuzaliwa kwenye familia yao pia, na ndio huko huko Kaini alipojitwalia mke.

**SWALI:** Kama KAINI alitwaa mke ambae alizaliwa na Adamu na Hawa ambao ni wazazi wake kwahiyo alimuoa dada yake je, kwahiyo ni halali kumuoa mwanamke ambae ni dada yangu wa damu?”.

---

**JIBU:** Kumbuka hata Adamu mwenyewe hakwenda kumtwaa mke kutoka kwenye familia nyingine, bali katika ubavu wake mwenyewe, hivyo kama ni undugu basi Adamu na hawa wana undugu mkubwa zaidi ya Dada na kaka...

Unaona? Mungu aliruhusu iwe hivyo mwanzoni kwa ajili ya uzazi, ili watu waongezeke, lakini baadaye Mungu alitoa maagizo kuwa ni makosa mtu kutwaa ndugu wake wa karibu na kumfanya kuwa mke wake..

*Mambo ya walawi 18:6 “Mtu ye yote aliye wa kwenu asimkaribie mwenziwe aliye wa jamaa yake ya karibu ili kumfunua utupu; mimi ndimi Bwana”.*

Na pia mstari wa 9 unasema...

*9" Utupu wa umbu lako, binti ya baba yako, au binti ya mama yako, kwamba alizaliwa nyumbani mwenu au kwamba alizaliwa kwengine, utupu wa hao usifunue".*

Kwahiyo ni machukizo kuoia ndugu yako yoyote yule wa karibu.

**Ubarikiwe**

**Jiunge na magroup yetu ya whatsapp kwa kubofya hapa >  
Group-whatsapp**

---

**Mada Nyinginezo:**

**MTI WA UZIMA NA MTI WA MAARIFA.**

**UZAO WA NYOKA.**

**SIKUKUU 7 ZA KIYAHUDI ZINAFUNUA NINI KWETU?**

JE! Kaini alimpatia mke wake wapi?

**IMANI NI KAMA MOTO.**

**SAUTI AU NGURUMO?**

**RUDIA, TENA NA TENA KUMWOMBA MUNGU USIKATE TAMAA.**

---

**Rudi Nyumbani:**

Share on:  
WhatsApp

[Print this post](#)